*SWAHILI FORUM 11 (2004): 69-73*

# JAZANDA YA NJOZI KATIKA BAADHI YA MASHAIRI YA EUPHRASE KEZILAHABI

# (ONEIRIC IMAGES IN EUPHRASE KEZILAHABI'S SELECTED POEMS)[1]

GRAZIELLA ACQUAVIVA

This article is based upon the following concept: Poetry is a chain of representation of the sub-conscience that is the creative source. We can read the poetic text in many ways, but if we imagine the text as the stage of images, we can understand the fundamental abstraction of the conscience. In this sense, oneiric images in some of Euphrase Kezilahabi's poems will be analysed by using insights from psychoanalytic theory.

Euphrase Kezilahabi amejulikana sana katika fasihi ya Kiswahili ya siku hizi kama yule mshairi aliyetumia sana – zaidi kuliko washairi wengine – ushairi huru ulioleta mgogoro mkubwa katika miaka sabini na themanini.

Katika diwani zake mbili zinazoitwa *Kichomi* (1974)[2] na *Karibu Ndani* (1988)[3] tunakuta maswala mbalimbali ya kijamii, ya kisiasa na ya kisaikolojia ambayo ni ya kawaida katika fasihi ya Kiafrika ya siku hizi, lakini mshairi huyu ni mtunzi wa pekee kwa jinsi yake ya kutumia sitiari na mafumbo.

Njozi za ulimwengu zinazojitokeza katika ushairi wa Kezilahabi zinafanana sana na zile za mtu anayeweweseka akiwa usingizini. Njozi hizi ni kama maonyesho ya fujo ya kutoka ndani, na ukengeuko wa binadamu.

Katika shairi la *Wimbo wa Mlevi* tunasoma:

*Kama Mungu angewauliza wanadamu*
*Wanataka kuwa nani kabla ya kuzaliwa,*
*Hilo ndilo lingekuwa swali gumu maishani.*
*Na watu wangeishi kujutia uchaguzi wao.*
*[...]*

---

[1] Makala yalitolewa katika kongamano la kumi na saba la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Bayreuth, tarehe 30 Mai hadi 1 June 2004.

[2] Euphrase Kezilahabi. 1974. *Kichomi.* Nairobi – Lusaka – Ibadan: Heinemann.

[3] Euphrase Kezilahabi. 1988. *Karibu Ndani.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

*Wote wangetamani kuwa kinyume cha walivyo.*
*Sijui nani angekuwa nani.*
*Lakini mimi mlevi ningependa kuwa ye yote*
*[…]*
(Kezilahabi 1974: 64)

Katika utafiti wake wa kishairi, Kezilahabi anayatazamatazama mazingira na mambo ya dunia, na tena kwa makini… picha zake za malimwengu na ubinadamu zinaeleza, kwa upande mmoja, mambo yalivyo na, kwa upande mwingine, mambo yajitokezavyo ndotoni.

Mshairi huyu anatuonyesha picha zake akitumia vitu, miti na mengineyo kama mambo yenye hisia, vile vile mambo haya yanapatikana katika fasihi ya simulizi.

Mfano halisi ni *Ngoma ya kimya*:

*[…]*
*Lakini labda miti hii michache yakumbuka*
*[…]*
*Nao upepo ukinifundisha lugha ya kimya*
*[…]*
(Kezilahabi 1988: 43)

Jinsi hiyo ya kutunga ushairi inatuonyesha pia mtu-mshairi ambaye anajua vizuri mambo ya dunia na mahali anapokaa, lakini, wakati ule ule anaendelea kutafutatafuta Ego yake kwa busara kama katika shairi la *Wanadamu Tunawajueni* anapoandika:

*Mimi ni nguo ya ulimwengu*
*Huvuliwa nikawekwa pembeni*
*[…]*
*Mimi ni sabuni ya Ulimwengu*
*Nimepapasa miili ya watu wengi*
*[…]*
*Mimi ni chakula cha Ulimwengu*
*Nimepapaswa na ndimi nyingi, nimeumwa.*
*Nimekaa ndani ya matumbo kila aina*
*Yaliyokwanyuka na pengine nilielea*
*Mwenye bia pengine hukumbana na tegu.*
*[…]*
(Kezilahabi 1974: 61)

Inawezekana kutambua ulinganifu fulani kati ya ushairi wa Kezilahabi na utafiti wa Ego ambao amefanya Carl Gustav Jung wakati alipokuwa akisikia upweke maishani mwake: yeye hakuwakimbilia watu wala dini, lakini aliangaliaangalia picha za kibinadamu zinazojitokeza katika njozi

zake. Kwa hiyo alianza safari yake ya kutoka ndani, kama inavyodhihirika katika wasifu wake Jung. Humu tunasoma:

> "Kwa ajili ya kuelewa mazingaombwe yangu, nilijikuta mara nyingi kwenye mteremko mkali […] Ilikuwa kama safari ya kwenda mwezini, au nilikuwa kama nikiteremka hadi pangoni […], ilikuwa inaonekana kama nipo ahera […]" (Jaffé 1978: 223)

Katika shairi la Kezilahabi linaloitwa *Hii Moja Hadithi* upweke unaomsumbua mshairi unarudi nyuma ukipita njia zote za roho yake kama ndotoni ambamo picha na kumbukumbu za maisha ya kibinadamu kama, kwa mfano, wakati wa kuzaliwa, zinachanganyika na picha za kifantasia:

> *[...]*
> *Ujana wangu ulianza kwenye ua waridi fumbo,*
> *Ukaishia kwenye gamba kandokando ya mto,*
> *Baada ya kisu kutokata kamba niloning'inia.*
> *Nimepanda vilima na kushuka hadi pangoni,*
> *Nikaselea magofuni karibu na kisima cha uzima.*
> *[...]*
> (Kezilahabi 1988: 45)

Maji yamekuwa kama kioo kinachotupa mambo mbalimbali ya Ego iliyobadilika, kama tunaweza kuona vile vile katika shairi la *Mto wa Haki*:

> *[...]*
> *Pole pole alianza kujiona mjinga kwa kuogopa*
> *Maji yaliyokuwa yakimtakasa mwenzake.*
>
> *[...]*
> *Alisikia sauti ya haki na usawa wa binadamu:*
> *kwa mda wa dakika moja alielewa ukweli*
> *Ambao vitabu vyote vilikuwa vimeshindwa kumweleza.*
>
> *Alikuwa ameona kivuli chake majini.*
> *Unafanya nini? Sauti iliuliza.*
> *Hakuweza kujibu: mwili wake ulikuwa umeganda*
> *[...]*
> (Kezilahabi 1974: 17)

Tena katika shairi hili, binadamu anaonekana kama mtu aliyeshikwa na mashurutisho ambayo hayaeleweki, hayaonekani au yale yaliyo dhahiri na yanayomhangaisha sana; binadamu huyo hayakimbii mashurutisho hayo kwa sababu anajua vizuri kwamba utakuja wakati ambapo kila binadamu lazima akabili haja ya kupata kujua Ego yake binafsi akizingatia kila kitu kinachotoka ndani yake.

Katika *Hii Moja Hadithi*, kama alivyofanya Jung zamani, Kezilahabi pia anazungukazunguka njia zote za nafsi yake:

> *[...]*
> *Nimeuona ule mji wenye lugha ya kimya,*
> *Nao huo mto wa damu ilimopotea miswada.*
> *Nimeshuhudia pia utapikaji wa roho,*
> *Na jinsi zilivyopotea kwenye maji ya uzima.*
> *Nimeicheza usiku kucha ngoma ya vurumai.*
> *[...]*
> (Kezilahabi 1988: 45)

Ndoto ina maana ya mawasiliano kati ya wakati wa kale na ule wa kisasa, pamoja na kuwa kama tamthiliya ya maisha halisi; ndoto inaweka jukwaani ovyo nyakati na kumbukumbu mbalimbali ambazo nje ya ndoto zingetambuliwa na binadamu kama ishara za fujo.

Wakati ambapo Jung alisafiri mahali palipoitwa naye 'ahera', aliwakuta babu zake wa kiroho, mmoja wao alikuwa Filemone. Kezilahabi pia anasikiliza sauti ya babu yake inayotoka ndani yake mshairi kama tunavyoweza kusoma katika shairi la *Nimechoka*:

> *[…]*
> *Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa*
> *Katika shamba la mawele, na mwenye shamba*
> *Huvuta waya kutoka nyumbani, itingishike kuwatisha ndege.*
> *[…]*
> *Sauti ya baba inasema kwa msisitizo*
> *"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka,*
> *Lakini endelea kushikilia hiyo waya*
> *Kama unazo nguvu bado, na usikate tamaa,*
> *Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa,*
> *Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,*
> *Nawe kudondoka, utadondoka!*
> *[…]*
> (Kezilahabi 1974: 34; 35)

Tukiyafikiria maisha ya kibinadamu kama yanayoyumba kati ya kuwako na kutokuwako, maisha hayo yanaonekana hayana nguvu.

Njozi zinafaa tuelewe, kwa maana ya kisitiari, zile nguvu za *Uwezo* ule uliokuwa unaonyeshwa na *Kifo* na *Wakati*. Mambo haya yanaweza kufahamika kwa lugha maalum ambayo Erich Fromm (1900-1980), mwanasaikolojia wa Kijerumani, aliita 'lugha maalum iliyosahaulika', yaani lugha ya sitiari.

Katika lugha hii, inawezekana kuupata uhusiano kati ya neno na ndoto. Tena, ndoto ni kama ile daraja ambayo washairi na wenye kuota wanasafiri ili wafike mahala pasipo mwanzo wala mwisho.

Kuhusu picha mbalimbali zinazojitokeza ndotoni, Hillman 1988 anazishughulikia zile za wanyama. Yeye anaeleza kwamba picha za hawa wanyama ndotoni zinafasiriwa kama maonyesho ya sehemu ya silika ya tabia ya kibinadamu.

Maelezo haya yanatokea nadharia ya Darwin ijapo inaonekana kwamba Hillman (1988: 139-141) anapenda zaidi kuzifikiria picha za wanyama kama *'totem'* au kama mizimu inayotusaidia wakati ambapo tupo kizani.

Katika *Kisu Mkononi* tunasoma:

*[...]*
*Mbele chui mweusi, nyuma mwanga*
*Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi.*
*[...]*
*Sasa kama Simba-Mtu shauri nimekata.*
*Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili.*
*Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka*
*Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,*
*Kila mpigo wa moyo wangu*
*Huu mpigo muziki wa maisha.*
(Kezilahabi 1974: 13)

Kwa makala haya nimechagua mashairi machache lakini ya kutosha – natumai - kwa kuelewa maana ya mabadiliko na maendeleo ya ile lugha maalum iliyosahauliwa: kama tunavyoweza kuona, kila ishara inapata kuwa picha ya kila fikra ambazo zinajificha katika ukweli wa maisha na Kezilahabi ana nguvu na ujasiri wa kuzifunua fikra zake, lakini lazima tuseme kwamba kila kitu kinawezekana kwa sitiari na kwa ushairi.

## Marejeo

Cancrini, T. 1981. *Psicoanalisi Uomo e Società.* Roma: Editori Riuniti.

Hillman, J. 1984 [1983]. *Le storie que curano* [*Healing Fiction*]. Milano: Cortina.

Hillman, J. 1988 [1979]. *Il sogno e il mondo infero* [*The Dream and the Underworld*]. Milano: Il Saggiatore.

Jaffé, A. (Ed.). 1978. *Ricordi*, *sogni*, *riflessioni di C. G. Jung.* Milano: Rizzoli.

Kezilahabi, Euphrase. 1974. *Kichomi.* Nairobi – Lusaka – Ibadan: Heinemann.

Kezilahabi, Euphrase. 1988. *Karibu Ndani.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.